

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



Aprili 08, 2022

OFISI YA MKUU WA WILAYA,  
S.L.P 02,  
LUDEWA.

**TAARIFA KWA UMMA**

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Adrea Tsere leo Aprili 08, 2022 amemkabidhi Mwenge wa Uhuru wa Mwaka 2022 Mkuu wa Mkoa wa Njombe Waziri Kindamba Waziri, zoezi hilo la makabidhiano limefanyika katika Tarafa ya Masasi Wilayani Ludewa ambako ndiko Mwenge wa Uhuru ulikesha na kuzindua Miradi mbalimbali.

Ikumbukwe kwamba Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2022 zilizinduliwa rasmi Aprili 02, 2022 na kuanza rasmi kukimbizwa katika Halmashauri za Mkoa wa Njombe na hatimaye jana Aprili 07, 2022 mbio hizo zimemaliza kimkoa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa

Mara baada ya kuupokea mwenge huo Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Njombe Waziri Kindamba Waziri kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Ludewa amemkabidhi Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mwenge wa Uhuru wa Mwaka 2022 na makabidhiano hayo yamefanyika katika Wilaya ya Nyasa Mkonni Ruvuma.

Aidha Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2022 Ndg.Sahili Nyanzabara Geraruma wakati akimuaga Mkuu wa Mkoa wa Njombe amesema kuwa Mwenge wa Uhuru kwa Mwaka 2022 umeziangazia Wilaya zote za Mkoa wa Njombe kwa kukagua Miradi mbalimbali pamoja na kutoa elimu ya mambo mbalimbali ikiwemo kuhamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa pindi zoezi hilo litakapo anza, na akaongeza kwa kumpongeza na Mkuu wa Mkoa wa Njombe kwa kuendelea kusimamia vyema fedha za miradi yote ya maendeleo mkoani hapo na kumtaka kusimamia kwa wakati mambo yote yaliyo elekezwa kutekelezwa wakati mwenge huo ukipita kwenye Wilaya hizo.

**Chrispin B.Kalinga**  
**Afisa Habari (W) Ludewa**